**2**

# MAKUBALIANO YA KUPANGISHA SEHEMU YA BIASHARA (VYUMBA/CHUMBA)

## UKUMBI WA IDYDC - 2025

Makubaliano haya yamefanywa kati ya Iringa Development of Youth Disabled and Children – Care (IDYDC).

| PICHA PPs 1 |
|---|
| MPANGAJI |

Na

AURICAIR SERVICE wa S.L.P 336 MWANZA (Mpangaji)
Simu 0782012345

### SEHEMU YA I

Mkataba huu wa upangaji umefanyika baada ya pande zote mbili kuridhia na kukubaliana na masharti ya mkataba huu baada ya kuusoma na kuuelewa vizuri kwa ujumla bila ya kuacha kipengele hata kimoja kilichomo ndani ya makubaliano haya.

Makubaliano haya ni kuanzia tarehe 01/01/2025 hadi 31/12/2025.

### MALIPO:

a). Malipo ya chumba cha biashara jengo la ukumbi wa IDYDC kuanzia tarehe 01 Januari 2025 yatakuwa ni shilingi Laki moja na elfu themanini tu **(TSH 180,000/= )** kwa mwezi.

b). Malipo yote yanaweza kulipwa kwa awamu 2, awamu ya kwanza kuanzia tarehe 01 Januari 2025 hadi Juni 2025 (miezi sita) sawa na **TSH 1,080,000/=**, au **TSH 2,160,000/=** kwa mkupuo wa miezi 12 sawa na mwaka mmoja). Malipo ya awamu ya kwanza yanapaswa kulipwa wiki 2 kabla kuanza kwa mkataba huu, yaani kabla ya tarehe 01 Januari 2025.

c). Pia ifahamike kwamba kodi hii ya pango haijumuishi gharama za umeme, maji, uzoaji wa taka, ulinzi na usalama wa mali za mpangaji. Gharama hizi zitagharimiwa na mpangaji mwenyewe na sio vinginevyo. Malipo ya mlinzi kwa mwezi ni shilingi **20,000/=** na yatalipwa kila tarehe 25 ya mwezi.

STAMP DUTY PAID
Shs: 21,600
Receipt No: 9984120581352
Of: IDYDC
Signature: [signature]
For: Regional Manager Mwanza

Certified True Copy of the Original
Tumaini William Sanga
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths
Sign: Sanga
Date: 13/2/2025

**SEHEMU YA II**

**WAJIBU WA MPANGAJI:**

a) Pamoja na wajibu huu mpangaji atawajibika kulipa kodi ya pango kwa kadri ya utaratibu uliokubaliwa na pande zote, hivyo basi kushindwa kulipa kodi kwa utaratibu uliokubaliwa ni kukiuka masharti na makubaliano ya pande husika katika mkataba huu. Ukiukwaji unaweza kusababisha mkataba kusitishwa.

ii) Mpangaji atawajibika kutunza mazingira yote ya ndani na nje ya eneo kwa kadri ya maelekezo ya mpangishaji na kulingana na mandhari ya eneo husika.

iii) Pia ifahamike kuwa kama kutakuwa na hitilafu ya umeme imetokea katika eneo husika, mpangaji atawajibika kutoa taarifa kwa mpangishaji ili kupata idhini ya kutengeneza au kutatua tatizo hilo hatimaye kuepusha mafundi ambao wanaweza kutengeneza chini ya kiwango stahiki na kusababisha kuungua nyumba au mali za mpangaji/wapangaji.

iv) Kwamba endapo mpangaji atafanya matengenezo ya umeme bila kumhusisha mpangishaji na akasababisha hasara atapaswa kulipa fidia kwa watu wote ambao watakuwa wameathirika na tatizo hilo.

v) Kimsingi mpangaji ni vema awe na Bima ya biashara yake kwa kuwa mpangishaji hatawajibika kwa janga lolote linaloweza kujitokeza katika biashara yake.

vi) Mpangaji anatakiwa kudhibiti uingizwaji wa vitu vinavyoweza kusababisha milipuko ndani ya nyumba/eneo la biashara kama vile mafuta ya magari/petrol, baruti na pia haruhusiwi kufanya biashara haramu kama vile madawa ya kulevya ndani ya nyumba au mazingira ya eneo karibu na nyumba.

vii) Mpangaji hatoruhusiwa kufanya biashara haramu kama vile madawa ya kulevya ndani ya nyumba au mazingira karibu na eneo la nyumba. Kama mpangaji atakiuka matakwa ya kifungu hiki, mpangishaji atakuwa na mamlaka ya kuvunja mkataba na shitaka lolote linaweza kumkabili mpangaji na sio mmiliki wa nyumba.

viii) Pia ifahamike kuwa mpangaji hatoruhusiwa kupangisha eneo lolote la nyumba au chumba bila idhini ya maandishi kutoka kwa mpangishaji au wakala wake.

## SEHEMU YA IV

**KUVUNJIKA MKATABA**

Kwamba Mkataba huu unaweza kufika Mwisho kama mambo yafuatayo yatatokea wakati wa upangaji;

i. Kubadilika kwa sera na kuathiri biashara husika, hivyo pande husika zitakuwa na haki ya kufikia ukomo wa kuendelea na mahusiano ya kibiashara.

ii. Kutokea kwa majanga yasiyotarajiwa kama vile mafuriko, tetemeko la ardhi na majanga yanayoendana na hayo na kuathiri eneo la ofisi.

iii. Pia mpangishaji atakuwa na haki ya kuwaondoa kwa nguvu endapo mpangaji atakiuka vipengele vya mkataba huu na anakataa kuondoka kwa hiari katika nyumba.

***ANGALIZO:***

Kwa mwaka unaofuatia mpangaji utatakiwa kusaini mkataba mpya kadiri ya makubaliano na mpangishaji (IDYDC). Malipo ya pango yanaweza kubadilika kulingana na gharama za uendeshaji kupanda.

*Tafadhali zingatia maagizo hapo juu kinyume cha hivyo "Notisi" ya kusitisha Mkataba .azingatiwa.*

## SEHEMU YA V

**KUSAINI MKATABA**

Makubaliano haya yamefikiwa leo tarehe ........................na kusainiwa na pande zote mbili kama ifuatavyo:-

a). (Jina la mpangaji); AURIC AIR SERVICES LTD tarehe 3/2/2025

Sahihi [signature] Simu 0782012345



b). Mdhamini wako: (Jina) SELEMANI RASHID SELEMANI

Makazi yake: (Mtaa/Kata KIHESA, NGOME

Mkoa IRINGA anuani............................Simu 0716505734 tarehe 06/02/2025

c). Iringa Development of Youth Disabled and Children Care (IDYDC) (Mpangishaji);

Sahihi [signature] Cheo AFISA UTAWALA tarehe 12/02/2025

*(Mkataba huu baada ya kusainiwa urejeshwe IDYDC HQ ndani ya wiki moja)*

Stamp/mhuri

IRINGA DEVELOPMENT OF YOUTH DISABLED AND CHILDREN CARE
IDYDC
P. O. Box 795
IRINGA

Certified True Copy of the Original
Tumaini William Sanga
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths
Sign: Sanga
Date: 13/2/2025